**DAWA YAKO: Losartan Potassium ____mg**

**Kwanini ninapatiwa dawa hii?** Una shinikizo la juu la damu. Shinikizo la juu la damu ni hatari iwapo halitotibiwa. Linaweza kusababisha viharusi na mishtuko ya moyo. Unaweza kupoteza maisha kwa kuwa na shinikizo la juu la damu ambalo halijatibiwa. Kama una kisukari pia, dawa hii itasaidia figo zako kuepuka kudhurika kutokana na kisukari chako.

**Meza kidonge 1 mara tu baada ya kuamka kila siku.** Hauhitaji kula kitu kabla ya kumeza kidonge hichi.

**Nitajihisije nitakapokunywa dawa hii?** Nyakati nyingine, huwa kuna athari za kimatibabu zinazotokana na kunywa dawa hii. Athari ya kimatibabu ni jambo lile unaloweza kujihisi ambalo si la kawaida. Baadhi ya athari za kimatibabu zinazotokana na kunywa Losartan hutokea pindi mwili wako unapoanza kuizoea dawa hii na zinaweza kujumuisha kizunguzungu au kuwewesuka.

Baadhi ya athari za kimatibabu huwa hazitokei mara nyingi, hatahivyo zinaweza kuwa kali sana. **Piga 911 au tembelea Chumba cha Dharura upesi kama utajihisi kupata: mabaka ya ngozi; kuvimba kwa uso, mdomo au koo; kupata shida katika kupumua; ama, kuwa na kizunguzungu kikali.**

**Nini kingine ninachopaswa kufahamu?**

1. Unapaswa kunywa dawa hii kila siku hata pale utakapojihisi kuwa sawa.
2. Unapaswa kuijaza upya dawa hii kila mwezi.
3. Kama utatembelea ofisi ya daktari tofauti, kliniki tofauti ya kitabibu ama chumba tofauti cha dharura, utapaswa kuwataarifu kwamba una shinikizo la juu la damu na kwamba unakunywa dawa ya Losartan Potassium.

“Maudhui haya ni ya kwa makusudi ya utoaji taarifa pekee na hayapaswi kuhesabiwa kuwa kama ushauri wa afya wa kitaalamu. Daima tafuta kupata ushauri kutoka kwa Tabibu wako ama mhudumu mwingine wa afya mwenye sifa, kuhusiana na maswali yoyote unayoweza kuwa nayo yanayohusu hali fulani ya kiafya au matibabu.”